turathi zisizogusika

United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

KITENGO CHA TURATHI ZISIZOGUSIKA
www.unesco.org/culture/ich

TOLEO LA MESSENGER LA TURATHI ZISIZOGUSIKA

JUNI 2008 n° 9
ISSN 2071-7784





## Maafikiano 2003

YALIYOPITISHWA KUFIKIA MEI 21, 2008

1 ALGERIA
2 MAURITIUS
3 UJAPANI
4 GABON
5 PANAMA
6 UCHINA
7 JAMHURI YA AFRIKA YA KATI
8 LATVIA
9 LITHUANIA
10 BELARUS
11 JAMHURI YA KOREA
12 USHELISHELI
13 JAMHURI YA UARABUNI YA SIRIA
14 MATAIFA YA MILKI YA UARABUNI
15 MALI
16 MONGOLIA
17 CROATIA
18 MISRI
19 OMAN
20 DOMINICA
21 HINDI
22 VIET NAM
23 PERU
24 PAKISTAN
25 BHUTAN
26 NIGERIA
27 ICELAND
28 MEXICO
29 SENEGAL
30 ROMANIA
31 ESTONIA
32 LUXEMBOURG
33 NICARAGUA
34 CYPRUS
35 ETHIOPIA
36 BOLIVIA
37 BRAZIL
38 BULGARIA
39 HUNGARY
40 JAMHURI YA KIISLAMU YA IRAN
41 REPUBLIC OF MOLDOVA
42 JORDAN
43 SLOVAKIA
44 UBELGILJI
45 UTURUKI
46 BUKINI
47 ALBANIA
48 ZAMBIA
49 ARMENIA
50 ZIMBABWE
51 CAMBODIA
52 JAMHURI YA AWALI YA YUGOSLAV YA MACEDONIA
53 MOROCCO
54 UFARANSA
55 CÔTE D'IVOIRE
56 BURKINA FASO
57 TUNISIA
58 HONDURAS
59 SAO TOME AND PRINCIPE
60 ARGENTINA
61 UFILIPINO
62 BURUNDI
63 PARAGUAY
64 JAMHURI YA DOMINIKA
65 GUATEMALA
66 UHISPANIA
67 KYRGYZSTAN
68 MAURITANIA
69 UGIRIKI
70 LEBANON
71 NORWAY
72 AZERBAIJAN
73 URUGUAY
74 SAINT LUCIA
75 COSTA RICA
76 VENEZUELA
77 NIGER
78 CUBA
79 MONACO
80 DJIBOUTI
81 NAMIBIA
82 YEMEN
83 INDONESIA
84 MSUMBIJI
85 KENYA
86 ITALIA
87 BELIZE
88 SAUDI ARABIA
89 UZBEKISTAN
90 ECUADOR
91 GUINEA
92 GEORGIA
93 COLOMBIA
94 SRI LANKA
95 URENO

# Maelekezo ya Usimamizi wa Maafikiano kuhusu Ulinzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika

Katika kikao chake cha pili Kikuu kilichofanyika mnamo Februari 2008 huko Sofia, Bulgaria, Kamati maalum kati ya Serikali za Mataifa Wanachama ilikamilisha changamoto lake kuu la kwanza: utayarishaji wa mswada wa Maelekezo ya Usimamizi kwa lengo la kuongoza uwajibikaji wa Maafikiano. Hiki pia kilikuwa kikao cha mwisho cha uhusika wa sasa wa Kamati. Katika kikao cha pili kijacho (Juni 16 mpaka 19, 2008, Paris) Mkutano Mkuu unategemewa kuidhinisha Maelekezo ya Usimamizi na kuchagua wanachama wapya kumi na wawili kwenye Kamati hiyo.

Bi. Irina Bokova, Balozi na Mjumbe wa Kudumu wa UNESCO kutoka Bulgaria, aliongoza mkutano huo uliofanyika huko Sofia. Ni mkutano uliokuwa wa kikao cha nne na cha mwisho cha Kamati hiyo kuwahi kufanyika katika kipindi cha miezi 16 iliyopita, kwani mikutano ya awali ilifanyika huko Algiers, Chengdu na Tokyo. Katika vikao hivyo, Kamati ilizingatia pakubwa kuhusu Maelekezo ya Usimamizi, kupitia kwa ombi lililotolewa kwenye Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama. Kufuatia midahalo na kuidhinishwa kwa Maelekezo hayo ya Usimamizi na jopo la Mkutano Mkuu, Maafikiano hayo yataanza kutumika moja kwa moja. Katika kikao cha Sofia, Kamati ilisisitiza kuhusu Azma yake ya kwamba, sababu kuu ya kuwepo kwa Maafikiano hayo ni Kulinda – ikiwa ni kwa ushirikiano na, pamoja na kuwepo kwa wadau na wahusika wengine wa kimila. Kwa sababu hii, Kamati hiyo imehusishwa na umuhimu mkubwa wa

© UNESCO / David Stehl




*Mstahiki Bi. Irina Bokova (Bulgaria), Mwenyekiti wa Kikao maalum cha pili cha Kamati kilichofanyika huko Sofia.*

Ulinzi wa Dharura wa Orodha za Turathi Zisizogusika na vile vile katika uteuzi na utangazaji wa shughuli za kulinda zinazoambatana moja kwa moja na kanuni za Maafikiano hayo.

Suala kuu lililotawala ajenda ya kikao cha Sofia, lilikuwa ni kuhusika kwa jamii, vikundi vya kijamii, watu binafsi, vituo vya kiutafiti na asasi mbali mbali katika utekelezwaji wa Maafikiano. Halmashauri maalum ya ziada ya Kamati hiyo, ikiongozwa na taifa la Senegal, ilitayarisha mswada wa Maelekezo ya Usimamizi kuhusu suala hili na ambayo yaliwasilishwa kwenye Kamati, yakajadiliwa na kukubalika.

*(yaendelea Ukurasa wa 2)*

## Tahariri

Toleo hili la ' Messenger' linakuletea habari nzuri. Linashughulikia kikako cha hivi majuzi zaidi cha Kamati maalum kati ya Serikali za Mataifa Wanachama, wakati ambapo mswada wa Maelekezo ya Usimamizi wa Maafikiano ulipokamilika. Hata hivyo, Toleo hili' kwa sasa linapatikana katika lugha ya Kirusi, tunamshukuru sana mwenzetu Liubava Moreva aliye katika afisi za UNESCO huko Moscow. Tafsiri hii inazifikisha tano lugha zilizotumika katika matoleo haya. Mwisho kabisa, toleo hili linaelezea kwa kina miradi minne ya Ulinzi, inayoendeshwa katika maeneo na hali mbali mbali, na katika shughuli tofauti tofauti. Bila shaka kile kinachoifananisha miradi hii ya UNESCO, ni pamoja na umuhimu wa kudhihirika na kuwepo kwa hakikisho la kulindwa kwa mila na mioneko inayosimamia na kuashiria tamaduni na mila za jamii na watu katika jamii hiyo.

Wacha nikufahamishe kwamba Kitengo cha Turathi Zisizogusika kinatayarisha toleo la tatu lililohakikiwa la Ramani ya UNESCO ya Lugha zilizo katika Hatari ya Kuangamia. Toleo la mtandao litazinduliwa katika mwaka wa 2008 - Mwaka wa Umoja wa Mataifa wa lugha – huku toleo lililochapishwa likizinduliwa mnamo mwaka wa 2009. Hata hivyo, onyesho la Turathi-Hai: Kuzifikia Zisizogusika, zilizoonyeshwa katika ua wa Jengo la UNESCO la Fontenoy, linaweza kuonekana katika wavuti wa UNESCO wa 'ICH' wa http://www.unesco.org/culture/en/ich/expo/. Toleo la mtandao la maonyesho ambalo ni maalum kwa watu wasioona litazinduliwa hapo baadae.

*Rieks Smeets, Kitengo cha Turathi Zisizogusika*



*(yaendelea kutoka ukurasa wa 1)*

Maelekezo haya yanayofafanua kwa kina kanuni za 13 mpaka 15 za Maafikiano hayo, hushughulikia utekelezaji wa Maafikiano katika ngazi ya kitaifa. Muongozo fulani uliidhinishwa ili kuiwezesha Kamati hiyo kupanga kuhusika kwa watu waliotajwa hapo juu kwenye mikutano yao. Muongozo mwingine unayataka Mataifa Wanachama kushirikisha nyaraka za vipengee vya Turathi Zisizogusika zilizoko katika maeneo mengine ya Mataifa Wanachama, kwa lengo la kuzifanya Turathi hizo zifikie jamii husika.

Kati ya masuala yanayoleta kizungumkuti zaidi ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya vito 90 katika Orodha ya Wakilishi. Vito hivyo vilipatikana kati ya mwaka wa 2001 na 2005 – hususan suala la vito hivyo vilivyopo kwenye mataifa ambayo bado sio wanachama wa Makubaliano haya. Kamati hiyo ilithibitisha kwamba vito vyote vya thamani vilivyopatikana vitaorodheshwa moja kwa moja na kwamba haki na masharti yaliyopo, hayawezi kutenguliwa ama kufuatwa kando kando. Mataifa ambayo si Wanachama wa Maafikiano haya, yatakaribishwa ili kukubali haki hizi na kuanza kuyafuata masharti hayo. Ikitokea kwamba Taifa ambalo si Mwanachama linakiuka ama linashindwa kufuata masharti hayo, Kamati hiyo itakuwa na mamlaka ya kuondoa vito vya thamani vya Taifa hilo vilivyo katika Orodha Wakilishi.

Masuala mengine yaliyojadiliwa na Kamati hiyo yalihusu kuidhinishwa kwa mashirika yasiyo ya kiserikali na pendekezo la kutumia Hazina ya Maafikiano kwa miaka miwili ijayo. Kamati hiyo pia ilihusika katika ubadilishanaji wa mawazo kuhusu matumizi ya nembo ya Maafikiano hayo.

Kamati hiyo pia ilirekebisha Masharti yake ya Utendakazi, ili kugawa majukumu yake kwa wahusika wa Afisi yake na kuthibitisha kwamba wahusika hao wa Afisi hiyo watakutana katika Makao Makuu ya UNESCO, wakati wowote ule itakapoona pana haja ya kukutana hata ikiwa ni katikati ya vikao vya Kamati.

Masuala mawili muhimu ya mkutano wa mwisho yalihusisha kuletwa pamoja kwa Maelekezo yote ya Usimamizi yaliyotayarishwa katika vikao vitatu vilivyotangulia vya Kamati, na kufanya nyaraka moja na ripoti ya shughuli za Kamati. Nyaraka zote mbili zitawasilishwa katika Mkutano Mkuu ujao utakaofanyika mwezi Juni.

Mkutano huo uliohudhuriwa na Mataifa Wanachama 50 na Mataifa 24 ambayo si wanachama wa mkataba huo, yaliendelea na moyo huo wa ushirikiano na utendakazi bora, vitu ambavyo vimekuwa ndio kama nembo ya Kamati hiyo tokea pale mwanzoni. Rais wa Bulgaria na waandalizi wa kongamano hili walifanya kila waliloweza ili kuhakikisha kwamba mkutano ulifaulu, na walikuwa na mipango kabambe ya kitamaduni.

## Mila za maigizo na ngoma za WaCocolo, kutoka Jamhuri ya Dominika

Mila za maigizo na ngoma za Wa-Cocolo zilikuzwa kwenye kipindi cha katikati ya Karne ya kumi na tisa katika jamii ya wafanyikazi wahamiaji wa Ki- Carribbean waliokuwa wazungumzaji wa Kiingereza na waliokuwa wamefika kwenye jamhuri ya Dominika. Jamii hii ilikuwa na mila na lugha za kipekee, ikaanzisha makanisa yake, shule, jamii yenye mshikamano wa kipekee na vituo vya kiusaidizi. Matumbuzo yao ya maigizo yalikuwa ndiyo njia za pekee za kuonyesha mila, muoneko na tamaduni zao. Mchanganyiko wa Muziki na Ngoma huifanya mila kuwa na mvuto hususan wa chimbuko la Kiafrika huku pakiwa na ongezeko la vipengee vya tamaduni kutoka bara Uropa, mara kwa mara kutoka katika mila na kanuni za Biblia.

Maonyesho ya maigizo ya Wa-Cocolo hufanyika nyakati za sherehe za Krismasi katika maadhimisho ya St. Peter's na pia katika hafla mbali mbali, huku vikundi vya wasanii wakitunga nyimbo na matumbuizo ya tamaduni tofauti tofauti, ikiwa ni pamoja na nyimbo za Krismasi, uzururaji, ama tambo na maonyesho ya ngano; kama vile 'Daudi na Goliati', 'Moko-Yombi', ama '*Cowboys and Red Indians*'.

Leo hii, kizazi cha Wa-Cocolo kimechanganyika vyema katika jamii ya Wadominika na wamesambaa nchini kote. Huku viongozi wa kijamii wakiendelea kuongea Ki-Caribbean-Kiingereza nyumbani kwao, wengi wao wanazungumza Kihispania. Mila pia zimetatizika pakubwa; pamebaki kikosi kimoja kinachojitahidi kuwafundisha vijana wa kizazi cha sasa kuhusu mila na tamaduni.

Afisi ya UNESCO ya Havana, inafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na wanachama katika jamii, ambao walianzisha mradi mdogo wa kuchangia katika ufufuaji wa mila zao. Kikundi hiki kinatazamia kuboresha kanuni za mafundisho kwa kuzitambua mila na kuimarisha usaidizi wa kifedha. Kilichokuwa muhimu sana katika mpango huo, ilikuwa ni mpango wa harakati za sherehe iliyofanyika kwa mara ya kwanza mnamo Desemba 2007 huko San Pedro de Macorís, eneo lenye historia ya miaka 200 tokea kuzaliwa kwa Cocolo. Sherehe hiyo, iliyofahamika kama *'Good Morning Wavaberry'* baada ya wimbo wa kimila wa Wa-Cocolo, iliangazia mchango mkubwa wa Wa-Cocolo katika tamaduni za Kidominika. Kadhalika ilitoa fursa kwa jamii ya Wa-Cocolo kujadili mikakati muhimu ya dharura ya kulinda mioneko ya tamaduni zao, na ilisaidia kutangaza katika ngazi za kitaifa. Hatua muhimu sana, hata ikawa, ndio usajili kamili wa jamii ya Wa-Cocolo, ambayo baada ya muda mrefu inaweza kuwalinda wasimamizi rasmi wa mila, na hali kadhalika kufahamika katika jamii ya Wadomonika.

**MUDA WA UTELEZAJI:** 2007-2008
**BAJETI:** Dola za Marekani 6,000 (Mradi wa Kawaida UNESCO)
**MSHIRIKISHI:** Victor Marín, *v.marin@unesco.org.cu*
(Afisi ya UNESCO iliyoko Havana)

### Maafikiano hayo yanahusisha Mataifa Wanachama na Mataifa yasiyo Wanachama kwa viwango sawa

Kwa mfano, mwanzoni mwa mwaka huu, mamlaka ya Jiji la Ufaransa la Rennes, ilimfanya Diwani wa Manispaa hiyo Bi. Ana Sohier kuwa mjumbe wa kwanza wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika, wakati ambapo Canada, Serikali ya eneo jipya la Labrador, ambayo imehusisha ulinzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika kama kipengee muhimu sana katika Mikakati ya Mpango wa Tamaduni, walimuajiri Dale Jarvis kama Afisa wa mkoani wa Maendeleo ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika.

La ziada ni kwamba, Bw. Dale Jarvis alisomea katika Chuo Kikuu cha Memorial University huko St. John, na wakati huu anashirikiana na Serikali kuanzisha mradi wa kuunda Orodha ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika za mkoa. Jukumu kamili la Serikali hiyo ni kuhakikisha kwamba Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Eneo Jipya la *'Newfoundland'* na Labrador zimehifadhiwa kama Turathi-Hai na chanzo cha ubunifu wa kijamii. Soma wavuti kupitia kwa http://www.arts.mun.ca/hypertext/websites/ich/resources/ICH_Strategy_Final_Draft-april.pdf

© Diego Féliz

(Kushoto). *Sherehe ya Kwanza ya Utamaduni wa Cocolo kwenye barabara za San Pedro de Macoris, Jamhuri ya Dominica.*

(Kulia) *Chifu Paul Tahi Hubwehubwen Vanua kutoka kisiwa cha North Pentecost, Rais wa Baraza la Kitaifa la Machifu wa Malvatumauri, akiwa amevaa pembe za nguruwe, mikeka ya pesa ya Bari memea na ushanga wa makombe, Port Vila, Septemba 2004.*

(Mbali kulia) *Maandamano ya tarehe 18 Novemba 2006 Port Vila ili kusherehekea azimio rasmi la Serikali ya Vanuatu mwaka wa 2007 kama "Mwaka wa Uchumu wa Kiasili".*



© Kirk Huffman




© Kirk Huffman

## Kulinda Michezo ya Wa-Afar na Wasomali katika Upembe wa Afrika

Michezo ya kiasili ya bao imekuwa kwa muda mrefu kama shughuli ya kupitisha wakati miongoni mwa jamii za wafugaji katika Upembe wa Afrika. Lakini uchezaji na upitishaji wa michezo hii sasa umekumbwa na tisho la ujenzi wa miji pamoja na athari za utandawazi. Kutokana na hali hii, Djibouti iliomba usaidizi kutoka kwa Shirika la UNESCO kupitia kwa mradi maalumu wa kulinda michezo hii mnamo mwaka wa 2007.

UNESCO ilikubali ombi hilo na ikazindua mradi huo wa kuhuisha michezo hii ya kiasili miongoni mwa marika yote katika jamii. Ilizingatia hasa upitishaji wa michezo ya bao kama vile *Bub, Riyo na Ka dhalis* miongoni mwa watoto wa Ki-afar na kisomali nchini Djibouti. Mradi huo ambao ulifadhiliwa kupitia kwa udhamini wa UNESCO pamoja na Hazina ya Ujapani, utaendelea hadi mwaka wa 2009.

Kituo cha Mafunzo na Utafiti (Center for Studies and Research) nchini Djibouti kilifanya utafiti wa nyanjani wa mradi huo katika sehemu mbalimbali nchini humo. Watafiti kutoka katika taasisi hiyo ya kitaifa waliwahoji wajuzi wa michezo hiyo, wakakusanya habari kuhusu desturi, majukumu na historia ya michezo hiyo. Tukio mojawapo la utafiti huu lilikuwa kuanzishwa kwa mfuko wa mitindo uliohusisha zana zote zilizohitajika ili kucheza michezo hiyo. Mfuko huo ulianzishwa na chama cha kiasili kiitwacho *Paix* na *Lait*. Aidha, kuna mipango ya kusambaza mfuko huo wa zana katika shule zote.

*Paix* na *Lait* pia kinatayarisha warsha katika shule. Mwishoni mwa mradi huu, wahusika wataweza kutathmini matokeo na kujadili mpango wa kulinda michezo hiyo ya Wa-Afar na Wasomali.

Mradi huu pia ambao unasimamiwa na Afisi ya UNESCO iliyoko Nairobi bado unaendelea, na umeweza kuongeza shauku ya watu ya kutaka kucheza michezo hiyo ya bao. Tarehe 31 Disemba mwaka wa 2007, wizara inayohusika na utamaduni ilifanya michezo ya kitaifa iliyohusisha michezo ya bao ya kiasili. Takriban wachezaji 120 walipambana hadi wakashiriki katika mashindano ya kimaeneo ambayo yalisambazwa na vyombo vya habari vya taifa.

Kutokana na mradi huu, Djibouti inapata tajriba nzuri ya kutambua, kuandika na kulinda sehemu mojawapo ya utajiri wa turathi zisizogusika za jamii mbalimbali zinazounda jamii pana ya nchi hiyo.

**MUDA WA UTELEZAJI:** 2007-2009

**BAJETI:** Dola 53,000 za Kimarekani (UNESCO/Japan Funds-in-Trust)

**MSHIRIKISHI:** Fumiko Ohinata, *f.ohinata@unesco.org* (UNESCO Nairobi)

© UNESCO / Fumiko Ohinata



*Onyesho la mchezo wa kiasili "Ri yo ka Dhalis" katika uzinduzi wa mradi Februari, 2007.*

## Benki za Kiasili za Pesa huko Vanuatu

Huko Vanuatu, vitu kama vile pembe za nguruwe, aina fulani za mikeka na makombe yaliyofumwa pamoja yana thamani mahsusi ya kitamaduni. Yanahusisha pia thamani ya kiuchumi kutokana na matumizi yao katika uchumi wa jamii, mbali na kumpa mtu sifa kijamii.

Katika mwaka wa 2004, kituo cha kitamaduni cha Vanuatu (Vanuatu Cultural Center) au pia *VKS, Vanuatu Kaljoral Senta,* kilizindua mradi uliohusisha kuupa nguvu na kuuendeleza mfumo wa benki usio wa kawaida uliohusisha vitu vyenye thamani ya kiasili badala ya pesa za kawaida. Chini ya usaidizi wa Afisi ya UNESCO ya Apia, wafanyi kazi wa nyanjani wa VKS ambao ni wa kujitolea, na ambao walikuwa wanajamii waliohamasishwa kushiriki katika mradi huu, walipewa vifaa kama vile nyua za nguruwe na nyaya ambazo zilisaidia kuwepo kwa nguruwe hao katika uchumi wao wa kienyeji. Watu waliweza kulipa kupitia vitu hivyo vya thamani ya kiasili. Athari iliyobainika ni kuwezesha kuwepo kwa uzalishaji wa vitu hivyo vya thamani huku vikichangia kuchechemua ongezeko la mapato na kuhuisha thamani na desturi za kiasili za watu wa Vanuatu.

Kwanza ukaguzi wa nyanjani ulitambua jamii ambazo zingefaidika kutokana na benki za kiasili. Hili lilifuatiwa na uimarishaji wa mikakati ya ukuzaji na uwekaji katika benki namna mbalimbali za utajiri wa kiasili. Mbali na kuanzisha benki za kiasili za pesa, kampeni ya kitaifa iliandaliwa ili kuhamasisha watu kuhusu majukumu na thamani za mitazamo hii ya kiasili kuhusu uchumi. Mnamo mwaka wa 2007, Serikali ya Vanuatu ilitangaza mwaka huu kuwa mwaka wa uchumi wa kiasili. Ilisherehekea azimio hili kupitia maandamano yaliyofanyika tarehe 18 Novemba, 2006 mjini Port Vila. Tukio hili lilidhibiti chumi za kiasili pamoja na kulinda ujuzi na desturi husika kupitia sera ya serikali.

Bidii ya VKS ilipelekea kufaulu kwa mradi huu. Kituo hicho cha VKS pia kilishirikisha machifu wa jamii mbalimbali pamoja na wawakilishi wa serikali katika ukuzaji na utekelezaji wa mradi. Aidha, kilitumia mtandao wake wa wafanyi kazi wa nyanjani kwa umahiri – chama ambacho kina mtandao mpevu zaidi Vanuatu, na chenye mtandao mpevu zaidi mashinani katika eneo la *Pacific,* na kwa hivyo kuweza kueneza mradi huo nchini kote. Mfano wa mtandao huo umeweza pia kuwasilishwa katika nchi zingine za *Pacific* ambazo huenda zikataka kuanzisha utaratibu kama huo kwa kuzingatia mageuzi yanayoafikiana na matakwa yao.

**MUDA WA UTELEZAJI:** 2004-2007

**BAJETI:** Dola 159,305 za Kimarekani ((UNESCO/Japan Funds-in-Trust)

**MSHIRIKISHI:** Mali Voi, *mali@unesco.org.ws* (UNESCO Apia)

MCHAPISHAJI Kitengo cha Turathi Zisizogusika
Sekta ya Tamaduni, UNESCO
1 Rue Miollis
75732 Paris Cedex 15, Ufaransa
Barua pepe: ich@unesco.org
Kipepesi: +33 (0) 145685752
MHARIRI MKUU Rieks Smeets
JOPO LA UHARIRI An-Heleen De Greef, Kaori Iwai, David McDonald, Maria Minana, Fumiko Ohinata, David Stehl

***Toleo la Messenger kuhusu Turathi Zisizogusika*** linapatikana katika umbo la chapa na elektroniki kwa Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Kiarabu na Kirusi (katika umbo la elektroniki).

Nakala ya Kiarabu imewezeshwa kupitia kwa mchango wa kifedha wa Mamlaka ya Utamaduni na Turathi ya Abu Dhabi, Milki ya Abu Dhabi – U.A.E.

Yote yaliyomo yanaweza kupakuliwa katika (www.unesco.org/culture/ich) na kupigwa chapa bila malipo ilimradi mwandishi atambuliwe.


© Conselho das Aldeias Wajãpi-Apina

turathi zisizogusika

## AJENDA 2008

**APRILI 10 – JUNE 10**
Onyesho la picha: "Turathi Hai: Kuchunguza Zisizogusika". Santo Domingo (Parque Independencia) and Ciudad de Santiago, Dominican Republic.

**JUNI 16–19**
Kikao cha pili cha Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama wa Maafikiano kuhusu Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika. UNESCO, Paris.

**JUNI 23–24**
Warsha: "Ujenzi wa Uwezo katika Utekelezaji wa Maafikiano ya 2003 kwa Mataifa Wanachama ya Kiafrika ya Maafikiano"UNESCO, Paris. Watazamaji kutoka katika mataifa mengine wanachama wanakaribishwa.

**SEPTEMBA 15 – OCTOBER 15**
Onyesho la picha: "Turathi Hai: Kuchunguza Zisizogusika" linaloonyeshwa katika Platia Eleftherias na katika barabara za Ledras et Onasagorou. Nicosia, Cyprus.

**NOVEMBA 4–8**
Kikao cha tatu cha Kamati maalumu kati ya serikali za Mataifa Wanachama kuhusu kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Istanbul, Uturuki.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na: *ich@unesco.org*

## *Shashmaqom* – Kulinda turathi ya kawaida

*Shashmaqom* ni muziki wa kiasili na wa kirasimi wenye kiwango cha juu cha ubora katika Asia ya Kati. Muziki huu wenye asili ya kimji, umekua zaidi ya karne kumi katika miji ambayo leo inahusisha Tajikistan na Uzbekistan. Aidha, unahusishwa na miji mikuu ya Bukhara na Samarkand.

Neno 'Shashmaqom' linamaanisha 'Maqom sita', ambapo maqom linahusisha uimbaji wa muziki unaojumuisha ala na sauti za binadamu. Muimbaji au waimbaji huchangiwa na lahani za banjo, fidla, ngoma na zumari. Waimbaji huanza na muziki wa ala kama utangulizi na kufuatiwa na nasr, ambao ni uimbaji unaohusisha aina mbili za nyimbo.

Muziki wa Shashmaqom huhitaji mafunzo mahsusi yaliyojengwa kwenye misingi ya upokezaji wa kimdomo kutoka kwa mwalimu kwenda kwa mwanafunzi kwa sababu uandishi huweza tu kurekodi mfumo wa kimsingi pekee.

Kutoka mwaka wa 1970 na kuendelea, wanamuziki wa Shashmaqom walihamia katika nchi za Israeli na Marekani. Baada ya kupatikana kwa uhuru kwenye mwaka wa 1991, Tajikistan na Uzbekistan zimechukua hatua za kulinda Shashmaqom, lakini ni wanamuziki wachache tu ambao bado wanatumia mitindo ya kiasili. Hii leo idadi kubwa ya wanamuziki ni wahitimu kutoka katika taasisi moja iitwayo *Tashkent Conservatory,* ambayo hutoa mafunzo ya jinsi ya kutunga muziki wa Shashmaqom.

Baada ya UNESCO kutangaza muziki wa Shashmaqom kama Kito cha Thamani mnamo mwaka wa 2003, hili lilifuatiwa na mradi wa miaka miwili ambao ulihusisha programu za mafunzo, masomo ya uzamili, utengenezaji wa ala za kiasili, utayarishaji wa rekodi, usaidizi wa maakaba na uchapishaji wa utafiti na rekodi za sauti. Kipengele muhimu cha mradi huu ambacho kilihusisha Afisi za UNESCO huko Tashkent na Almaty kilihusisha pia kushiriki kwa pamoja kwa Tajikistan na Uzbekistan katika Sherehe za Kimataifa za Wanamuziki wa Shashmaqom mnamo Novemba, 2006. Sherehe hizo zilifanyika Dushanbe, ambao ni mji mkuu wa Tajikistan. Wana sanaa kadha wa Maqom kutoka katika maeneo tofauti ya Tajikistan walitumbuiza, pamoja na uimbaji wa pamoja kati ya wana sanaa kutoka Tajik na Uzbek, huku wakifanya sherehe hizo kuwa tukio muhimu la malumbano ya kitamaduni na uelewa wa pamoja. Tukio hili lilienezwa na vyombo vya habari na kufuatiwa na majadiliano ya pamoja kuhusu kulinda muziki wa kimila wa Shashmaqom ambao pia uliwajumuisha wasomi, wanasanaa na watungaji kutoka katika nchi hizo mbili.

Mradi huo pia ulifaulu kuwaleta pamoja wana sanaa wa jamii ya Shashmaqom kutoka katika pande mbili za mpaka. Pengine hili litaweza kuendeleza mila hii ya muziki. Mradi pia ulisababisha ujumuishaji wa madarasa mbalimbali ya uzamili kuhusu sanaa ya utendaji na utengenezaji wa ala, huku kazi ya kurekodi na utoaji wa mafunzo vikiwa vimeanza katika vituo vya Tajik *National Conservatory* huko Dushanbe na Taasisi ya Utafiti wa Sanaa (Research Institute of Fine Arts) huko Tashkent (Uzbekistan). Mradi huu pia umechangia pakubwa katika uhuishaji na uundaji wa mitandao mipya ya asasi zinazohusika na ulinzi wa Shashmaqom pamoja na turathi zisizogusika kwa jumla.

**MUDA WA UTELEZAJ:** 2005-2008
**BAJETI:** Dola 218,456 za Kimarekani (UNESCO/Japan Funds-in-Trust)
**MSHIRIKISHI:** Yuri Peshkov, *y.peshkov@unesco.org*
(UNESCO Almaty)
Anna Paolini, *a.paolini@unesco.org*
(UNESCO Tashkent)


© Otanazar Mat'yakubov

***Mkuu wa Shashmaqom, Rustan Boltaev, anafunza mwanafunzi wakati wa darasa la uzamili lililotayarishwa wakati wa mradi.***